

.Home > Hekaya Za Bahlul Mwenye Busara > (53). Ulipaji Wa Deni

Mtu mmoja alinua kumchokoza Bahlul katika imani yake kuhusu Imam al-Mahdi (a.f.) na kudhihiri .kwake ili kueneza utawala wa *haqi na uadilifu* duniani kote

Katika kikao kimoja ambapo na Bahlul pia alikuwapo, alisema: "Ewe Bahlul! Je si wewe unaitakidi kuwa Imam wako wa 12 al-Mahdi (a.f.) atadhiihiri katika zama za mwisho wa dunia na ataleta utawala wa haki na uadilifu? Iwapo wewe u-thabiti juu ya itikadi hii basi nikopeshe dinar mia tano ambazo nitakupa ".wakati Imam wako atakapodhiihiri

Bahlul alimjibu: "Bila shaka hiyo ndiyo itikadi na Imani yangu na niko tayari kukukopesha hivyo lakini ni lazima unihakikishie kuwa wewe hautakuwa umegeuzwa kuwa mbwa au nguruwe! Iwapo utageuzwa, "?basi nani atakayelipa

Kwa kusikia hayo wote waliokuwapo wakaangua kicheko na yule mchokozaji akabung'aa asiwe na la .kusema. Bahlul alijiondokea

Source URL:

<https://www.al-islam.org/ar/hekaya-za-bahlul-mwenye-busara-amiraly-m-h-datoo/53-ulipaji-wa-deni>